

**BUNGE LA TANZANIA**

-----

**MAJADILIANO YA BUNGE**

-----

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 3 Desemba, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba  
Wimbo wa Taifa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 33(1), napenda kutoa taarifa kwamba, katika Mkutano wa Kumi na Tatu, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (*The Constitutional Review Amendment Bill, 2013*). Kwa Taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, Muswada huo umekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria iitwayo Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Na. 9) ya Mwaka 2013 (*The Constitutional Review Amendment Act (No. 9) of 2013*). Kwa hiyo, Muswada ule ni Sheria kamili. (*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

**Muundo wa Mamlaka ya CDA**

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE)** aliuliza:-

Katika Bunge la Tisa Waziri Mkuu alitoa ahadi Bungeni kuwa Serikali itafanya mchakato wa kukusanya maoni kwa Wananchi kuhusu Muundo wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA):-

(a) Je, mpango huo uliishia wapi?

(b) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo ili Wananchi wapate fursa ya kueleza iwapo wanaridhia utendaji wa CDA au la?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU  
(SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuwahi kutoa ahadi ya kukusanya maoni kwa Wananchi kuhusu Muundo wa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (CDA). Kumbukumbu tulizonazo zinaonesha kwamba, katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2008/2009, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliahidi kuwa, Serikali itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu uamuzi wa kuhamisha Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, kwa lengo la kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya kutambua rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, imeshaitisha vikao viwili kwa ajili ya kupata maoni ya kuwawezesha kutunga Sheria mpya ya kutambua rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali. Kikao cha kwanza kilifanyika tarehe 19 Oktoba, 2012, katika Ukumbi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Dar es Salaam, ambacho kiliwahusisha wadau kutoka Wizara mbalimbali. Kikao cha pili kilifanyika tarehe 2 Februari, 2013, katika Ukumbi wa Hoteli ya St. Gaspar Dodoma, ambapo Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, walishiriki katika kikao hicho. Wajumbe wengine walioshiriki walitoka kwenye Taasisi za Serikali, Vyama vya Siasa, Taasisi za Dini, Asasi zisizokuwa za Serikali, Wawakilishi wa Wafanyabiashara pamoja na Wazee wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maoni yaliyokusanywa katika vikao hivyo nilivyovitaja, tayari Serikali imeshaandaa Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi ya kutunga Sheria mpya ya kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bura, swali la nyongeza!

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. FELISTER A. BURA]

(i) Kwa kuwa Serikali iliahidi kuandaa *Master Plan* ya CDA kwa sababu *Master Plan* iliyopo ni ya tangu mwaka 1973 CDA ilipoundwa na mpaka sasa inatumia *Master Plan* hiyo ya zamani; na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba *Master Plan* ya CDA itaandaliwa mapema iwezekanavyo ili Mji wa Dodoma uweze kupangwa vizuri na Makao Makuu yawe kati ya Wilaya ya Chamwino na Manispaa. Je, ni lini Serikali itafanya hiyo kazi ya kuandaa *Master Plan* ya CDA?

(ii) Kwa kuwa Wananchi wa Tanzania wamesubiri suala la Serikali kuhamia Makao Makuu ya Dodoma kwa muda mrefu; na kwa kuwa Serikali inasema inakusanya maoni ya Watanzania kujua kama Serikali ihamie Dodoma au isihamie Dodoma. Je, Serikali ipo tayari kukamilisha kazi hiyo ya kukusanya maoni ya Wananchi kabla ya mwaka 2015?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bura, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dodoma, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli CDA ilialika Wataalam Waelekezi, kuandaa *Master Plan* mpya, ambayo imeshaandaliwa tayari na kampuni moja kutoka South Korea wakishirikiana na Watanzania. Jana kwenye Kikao chetu cha Bodi tumeipitisha rasmi na nataka kuahidi kwamba, tutaikabidhi na kwa wakati ufao tutawaonesha hata Kamati inayohusika ya Bunge waweze kuona *Master Plan* mpya ya Mji wa Dodoma, ambayo sasa imeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, la pili, kama nilivyosema ni kwamba, tunakusanya maoni tuweze kutunga Sheria. Hivi sasa hatuna Sheria, lakini tunataka kutunga Sheria na Bunge lako litahusika katika utungaji wa Sheria ambayo itatamka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU  
(SERA, URATIBU NA BUNGE)]

rasmi kwamba, Makao Makuu ya Serikali ni Dodoma. Kwa hiyo, sasa hivi tupo katika *process* ya Kiserikali na utaratibu wa kukusanya maoni umeshapita, lakini kutakuwa na awamu ya pili ya kutafuta maoni ya Wadau kupitia Kamati za Bunge pindi utakapoletwa huo Muswada. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, aamini tu kwamba, Sheria tunaikimbiza kimbiza katika utaratibu wa Serikali na *Inshallah*, inaweza ikafika kabla ya muda waliopendekeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Diana Chilolo!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma ni pamoja na kujenga nyumba za kisasa, kama wanavyoendelea sasa hivi wanapima viwanja na wanauza. Kwa kuwa viwanja hivi vinauzwa kwa bei kubwa sana, kiasi kwamba Wananchi wa kawaida hasa vijana wanaoanza maisha hawatamudu kuvinunua katika eneo hili la Dodoma. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama hizi?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampa pole sana kwa kufiwa na mama yake mzazi.

Pili, ni kweli *CDA* inasimamia *Master Plan* na inasimamia vilevile upangaji wa mji. Katika upangaji wa mji ni pamoja na upimaji wa viwanja. Sasa vipo viwanja vya bei kubwa, vya bei ya kati, vya bei ndogo na vya wawekezaji na wajenzi wa nyumba. Gharama hizi zinakuwa kubwa kwa sababu mara nyingine tunatumia wataalamu waelekezi binafsi wa kupima hivi viwanja.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU*  
*(SERA, URATIBU NA BUNGE)]*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hakuna eneo ambalo halina mwenyewe. Kwa hiyo, ili tupime viwanja lazima yale maeneo tuyatwae, tuliweke fidia stahili halafu ndiyo tupime viwanja. Kwa hiyo, kile kiwanja kitakuwa na bei ya fidia ambayo tayari tumeshaiweka, ndiyo maana inaongezeka, siyo kwamba *CDA* inatengeneza faida, lakini kutokana na zile fidia ambazo tunawalipa wale wenye mashamba na maeneo ambayo tunayachukua.

Mheshimiwa Spika, viwanja vipotevya kutosha na hivi sasa tumeanzisha utaratibu tunawakopesha watu waweze kulipa kwa muda. Tuliweka miezi mitatu, lakini nimetoa maelekezo kwamba, muda wa kulipa angalau uwe mwaka mmoja ili alipe kidogo kidogo, kwa kipindi cha mwaka mmoja, tunaamini mtu anaweza akalipa pesa zote za kiwanja.

Mheshimiwa Spika, tunafikiri lazima tuendelee kwa utaratibu huo, ili kupunguza tatizo lililopo katika miji mingine, ambayo haikupangika vizuri. Ninyi nyote ni mashahidi, Dodoma angalau kidogo, Mji umepangwa vizuri kutokana na usimamizi mzuri unaofanywa na *CDA*.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Moses Machali, atauliza swali hilo.

Na. 2

**Watumishi Wabadhirifu Kuhamishwa Katika  
Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ni sababu gani zinazoifanya Serikali kutowafukuza au kuwaachisha kazi watumishi wabadhirifu katika Halmashauri mbalimbali huku baadhi yao wakihamishwa kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kushughulikia masuala ya nidhamu kwa Watumishi wa Umma, umeainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba Nane ya Mwaka 2002 na Marekebisho yake kwa mujibu wa Sheria Namba 18 ya Mwaka 2007. Sheria hiyo pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Kanuni za Kudumu za Utumishi, Toleo la Tatu la Mwaka 2009, ndiyo misingi ya kushughulikia mashauri ya kinidhamu. Aidha, Sheria na Kanuni hizo zimeainisha vyombo vinavyopaswa kuchukua hatua, utaratibu wa kuendesha mashauri na utaratibu wa rufaa na vyombo vya rufaa kulingana na ngazi mbalimbali za Watumishi.

Mheshimiwa Spika, uhamisho wa Watumishi wa Serikali kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine, unazingatia masilahi ya Utumishi wa Umma na unalenga kuboresha utendaji kazi. Kwa sasa hakuna uhamisho wa adhabu na hivyo Mtumishi wa Umma mwenye makosa, atashughulikiwa pale alipo mpaka hitimisho la hatua za kinidhamu litakapofikiwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2006 mpaka 2013, Watumishi mbalimbali wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu, ikiwemo kufikishwa mahakamani, kuvuliwa madaraka na kuachishwa kazi. Jumla ya Wakurugenzi 52 wa Serikali za Mitaa wamechukuliwa hatua na Watumishi wa Kawaida wa kada mbalimbali 814 wamechukuliwa hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali, swali la nyongeza!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kuwa, sijaridhishwa na majibu ambayo yametolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la Sheria ambazo zinaainishwa na Serikali zinajulikana, ni jambo jema kwamba, Sheria zipo. Tatizo la msingi inaonekana kunakosena uadilifu miongoni mwa mamlaka za kuweza kuchukua nidhamu ili kuwashughulikia Watumishi wote ambao wame-*demonstrate* vitendo ambavyo ni kinyume kabisa cha matarajio ya Wananchi.

(i) Je, Serikali inatoa msimamo gani mamlaka mbalimbali ambazo wakati mwingine zimeshindwa kuwachukulia nidhamu watumishi ambao wamefanya vitendo ambavyo vipo kinyume kabisa na utaratibu wa Sheria zetu hapa nchini?

(ii) Kwa kuwa upo ushahidi kwa baadhi ya Watumishi ambao wametolewa kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine; kwa mfano, aliyekuwa *Acting DMO* katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu alitolewa Kasulu na kupelekwa Wilaya moja huko Mkoani Iringa. Aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyuwi aliwahi kulalamikiwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao tupo nao ambao barua zao ninazo na zimeziwasilisha TAMISEMI, alitolewa Uyuwi na kuletwa Kasulu ambapo pia hali ni mbaya. Serikali inatoa kauli gani na ipo tayari kushirikiana na mimi wakati mwingine ili kuweza kuthibitisha haya na pale itakapobainika hatua za nidhamu ziweze kuchukuliwa pamoja na watu wengine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Moses Joseph Machali, kama ifuatavyo:-



## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)]*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, kwamba, kuna mamlaka ambazo zimeshindwa kutimiza wajibu wake. Mamlaka za nidhabu zimewekwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu na kama zimevunja Sheria, inabidi tufuate Kanuni, Taratibu na Sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe Wabunge. Tukiona mamlaka fulani halfai, ni vyema tukaleta Bungeni tukabadilisha Sheria zetu. Kwa Sheria za sasa hivi, mamlaka ambayo inashindwa kutimiza wajibu wake huwezi kuichukulia tena hatua za kinidhamu ile mamlaka.

Kwa hiyo, tunapowafukuza watu au tunapowaachisha, mimi nashauri kwamba, taratibu zifuatwe, badala ya kutumia siasa kuwafukuza watu au kuwaachisha, tuhakikishe tunachukua hatua za kinidhamu.

Mfanyakazi yeyote huwezi kumfukuza kienyeji, lazima ufuate Sheria, usipofuata Sheria haiwezekani. Hata wenzetu CHADEMA juzi juzi wametaka kumchukulia hatua za kinidhamu Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, wameandika kwanza makosa yake ili ajibu na baadaye wanaweza wakamchukulia hatua za kisheria. Kwa hiyo, lazima tufuate Sheria kwa Watumishi wa Umma na Wanasiasa pia tunafanya hivyo hivyo. *(Makofi)*

Swali la pili la Mheshimiwa Machali kuhusu Daktari aliyekuwa Kasulu; ni kweli Mheshimiwa Machali alikuwa na matatizo na Daktari huyo. Kwa jinsi walivyokuwa na misugvano na yule *DMO*, isingewezekana kukaa tena Kasulu. Yule bwana asingeweza kufanya kazi kwa jinsi walivyokuwa na msugvano na Dkt. Makusa. Kwa hiyo, Serikali *purposely* waliona wamhamishe wampeleke mahala pengine kama atakuwa na tuhuma aweze kurudi kujibu. Hali ilikuwa siyo nzuri mahali pale.

Kuhusu huyo *DED* anayemsema sasa hivi, jamani mamlaka za nidhamu zipo, kama kweli imethibitika kwamba yule Mkurugenzi ana matatizo, mimi nasema kwamba, hatua zinaweza kuchukuliwa. Mheshimiwa Machali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)]

alishatoa kilio hicho kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri ameunda Tume imeenda Kigoma tarehe 23 Oktoba, tayari imeshafanya uchunguzi na uchunguzi ule tunaufanyia kazi. Kwa hiyo, suala hili ameshalipeleka kwenye mamalaka husika. (*Makofi*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa kwenye Halmashauri zetu tuna Wakuu wa Idara; Utakuta Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari, Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi. Sasa tungeomba kujua hivi hawa Wakuu wa Idara katika kuhamishwa wanaohusika ni Utumishi, ni TAMISEMI au ni hizi Wizara kama Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kwa sababu kuonaonesha kidogo kama kuna mgongano? Tungependa kujua leo nani anahusika na kuhamisha hawa Wakuu wa Idara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)):** Mheshimiwa Spika, mhusika mkuu kwa mujibu wa Sheria anayetakiwa kuhamisha Watumishi wa Umma ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Baada ya kuzidiwa kazi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ime-*delegate*, yaani imekasimu madaraka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuwahamisha watumishi katika maeneo mbalimbali na TAMISEMI nao wame-*delegate* madaraka kwa ma-RAS kuwahamisha watumishi katika Mkoa husika.

Anayetakiwa kuhamisha ni Utumishi, lakini kutokana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa nyingi, tumekasimu madaraka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Kama watakuwa mame-*misuse* hiyo *power*, sisi Utumishi tunaweza tukarudisha madaraka yetu ya kuhamisha Wakuu wa Idara lakini tumekasimu sisi wenyewe.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, tumetumia dakika 20 kwa maswali mawili. Mheshimiwa Hezekia Chibulunje, swali linalofuata!

Na. 3

**Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino**

**MHE. HEZEKIA N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Serikali iliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuhamishia Ofisi zake kwenye Makao Makuu ya Wilaya hiyo huko Chamwino lakini mpaka sasa hawajafanya hivyo:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeiachia Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kufanyia shughuli zake Mjini Dodoma?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani lenye msukumo mpya kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuhamishia shughuli zake kwenye Makao Makuu yaliyoko Chamwino?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI))** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hezekia Ndahani Chibulunje, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilianzishwa, baada ya kugawanywa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma. Tangu kipindi hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imekuwa ikitumia Ofisi zilizokuwa zikitumika na Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma ambayo ni majengo ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuendelea kutumia majengo yaliyokuwa ya Halmashauri ya Wilaya Dodoma toka kuanzishwa kwake ni kutokana na kutokamilika kwa majengo ya Ofisi yake katika eneo la Makao Makuu Chamwino.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)]*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, jitihada kubwa zimeendelea kufanywa na Serikali kuhakikisha kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inahamisha shughuli zake katika Makao Makuu ya Wilaya ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inahamishia shughuli zake Makao Makuu ya Wilaya, katika kipindi cha mwaka 2010 mpaka 2014 kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 2.25 kimeshatumiwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi, ambalo ujenzi unaendelea hadi sasa na Jengo hilo lipo katika hatua ya kupaua ghorofa ya kwanza.

Kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kupitia maombi maalum na shilingi milioni 100 katika vyanzo vya mapato ya ndani. Hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imekwishachangia kiasi cha shilingi milioni 70 kwa ajili ya kukamilisha kazi mbalimbali. Hivyo, kukamilika kwa ujenzi wa Jengo hili kunategemea upatikanaji wa fedha za Serikali.

**MHE. HEZEKIA N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninataka kujua yafuatayo:-

(i) Waziri wa Nchi wa wakati huo, Mheshimiwa Mkuchika, alipotoa tamko la kuwaagiza Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kufanyia kazi zake Chamwino mara moja, ilijulikana wazi kabisa kwamba tangu Wilaya ianze, DC yuko Chamwino. Sasa nataka kujua kwa majibu haya Serikali inafuta maagizo yale ya Waziri?

(ii) Nataka nieleze kwamba pale Chamwino Ikulu kuna nyumba nyingi za Serikali ambazo zilijengwa katika utaratibu wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma, ambazo sasa hivi zimeshatelekezwa na zinaweza zikatumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. Je, kwa nini sasa hivi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HEZEKIA N. CHIBULUNJE]

agizo la Serikali lisikaziwe Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ihamie huko mara moja kutumia majengo yaliyopo wakati wakisubiri ujenzi unaoendelea? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chibulunje, kama ifuatavyo:-

Serikali bado haijafuta ile kauli yake ya Watumishi wa Chamwino kuhamia Makao Makuu, yaani pale Chamwino. Kwa sasa utaratibu unafanyika, Watumishi wote watumia Jengo la Mkuu wa Wilaya ifikapo mwisho wa mwezi wa Desemba mwaka huu. Kwa upande wa majengo, nyumba tatu zimeshakamilika ili Watumishi mbalimbali waweze kukaa. Kwa hiyo, lile agizo lililotolewa na Mheshimiwa Mkuchika, linatekelezwa na mwisho wa mwezi, Wafanyakazi wote Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, watahamia kwenye Jengo la Mkuu wa Wilaya na maandalizi yapo tayari.

Kuhusu kutumia majengo yaliyokuwa yamejengwa; yale majengo yalijengwa *purposely* kwa ajili ya Ikulu Ndogo na lile lengo halijafutwa; ndiyo maana ukiangalia kule Chamwino sasa hivi, majengo mengi yanafanyiwa ukarabati ili Mheshimiwa Rais anapokuja atumie Ikulu Ndogo ya Chamwino. Kwa hiyo, majengo yale yatatumika vilevile kama ilivyoahidiwa kwa ajili ya Ikulu Ndogo na si vinginevyo.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa Wilaya ya Bahi inatokana na kugawanywa iliyokuwa Wilaya ya Dodoma Vijijini na tayari Serikali ilishatoa agizo la Watumishi wote wa Halmashauri

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. OMAR A. BADWEL]

ya Wilaya ya Bahi kuhamia Bahi toka mwaka jana; kwa maana kwamba, ndipo watakapolipwa mafao yao ya uhamisho; na kwa kuwa kwa bahati nzuri Watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi wameshahamia Bahi na wanafanyia kazi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Bahi takriban mwaka umepita lakini hadi sasa bado wanaidai Serikali fedha zao za uhamisho. Sasa ni lini basi Serikali itawalipa fedha zao za uhamisho wale Watumishi waweze kufanya kazi vizuri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)):** Mheshimiwa Spika, ni kweli agizo la Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kuhamia Makao Makuu limeitikiwa na wale wafanyakazi wameshahamia Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, yaani Makao Makuu. Kuhusu masurufu yao, yaani *disturbance allowance* ya kuhamia kule Bahi, madai yao yameshakusanywa, yameshapelekwa Mkoani na Mkoani wameshapeleka Hazina, ni kati ya jumla ya madai mbalimbali ya Watumishi ambayo wanayadai kwa sasa hivi. Kwa hiyo, wawe na subira tu madeni hayo yatalipwa na Serikali.

Na. 4

### **Barabara ya Lami ya Kutoka Tanga Hadi Makurunge**

**MHE. OMAR R. NUNDU (K.n.y. MHE. SALEH A. PAMBA)**  
aliuliza:-

Katika kipindi cha mwaka 2010 – 2015 Serikali iliahidi kujenga kwa lami Barabara ya kutoka Tanga – Pangani – Makurunge (Bagamoyo):-

Je, ujenzi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (Bagamoyo), yenye urefu wa km 230 ni sehemu ya Barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ijulikanayo kama Malindi – Mombasa – Lungalunga – Horohoro – Tanga – Pangani – Saadan – Makurunge (Bagamoyo). Barabara hii kwa upande wa Tanzania kwa sasa inafanyiwa usanifu wa kina na Kampuni ya Kihandisi ya *Aurecon AMEI Limited* kutoka Afrika Kusini na kusimamiwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ufadhili wa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Upembuzi yakinifu wa Barabara hii ulikamilika mwezi Agosti mwaka 2012 na kazi ya usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza mara baada ya usanifu kukamilika na fedha za ujenzi zikipatikana. Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), imeonesha nia ya kugharamia Mradi huu kwa asilimia 50. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta wafadhili wengine kwa ajili ya kupata fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri.

Katika barabara hii kuna Mji wa Pangani ambao sasa hivi umefungika, haukuunganishwa na Miji mingine ya Mkoa wa Tanga wala haukuunganishwa na Miji mingine ya Tanzania na Dunia. Kwa nini katika utendaji huu na kwa kuwa fedha bado zinatafutwa na kilometa ni 230 ukilinganisha na kilometa 50 tu kutoka Tanga mpaka Pangani; Serikali haioni umuhimu wa kutoa kipaumbele kwa kipande kile cha Tanga – Pangani kwa sababu hizo ambazo nimezieleza kuhusu Pangani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuunganisha Tanga na Pangani na ndiyo maana tumeweka kwenye Mradi huu ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), inaendelea kuitengeneza Barabara hii kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika muda wote wa mwaka.

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2015 barabara nyingi ziliainishwa katika ujenzi wa barabara za lami na Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka jana nilipokuwa nikiuliza swali langu sambamba na swali kama linavyojainisha hapa, barabara ya kilometa 48 kutoka Kisarawe mpaka pale Maneromango ambayo imefanywa upembuzi yakinifu na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Novemba alipokuja Kisarawe kuahidi baadaye kitajengwa kwa kiwango cha lami.

Sasa kwa kipindi hiki kwa vile tupo katika mchakato wa bajeti; nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, ahadi ya Rais aliyoitoa kwa Wananchi wa Kisarawe na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2010 - 2015 kwamba barabara hiyo sasa mwaka huu inaingia katika bajeti ujenzi uanze mara moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafo, hata wewe unajua ni swali jipya kabisa kabisa, lakini Naibu Waziri kwa sababu ya ufundi wako naomba ujibu tu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwishaahidi kwamba, ahadi zote za Mheshimiwa Rais, ambazo amezitoea ndiyo mipango ya Serikali na tutaendelea kuiwekea bajeti kulingana na upatikanaji wa fedha. Fedha zikipatikana kwa mwaka unaokuja, basi tutaweka kwenye bajeti na kama haitawezekana basi mwaka utakaoendelea tutaweka kwenye bajeti. Kwa hiyo, vitu vyote inategemeana na upatikanaji wa fedha ili tuweze kutekeleza ahadi hizi za Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais.



Na. 5

**Upanuzi wa Barabara za Mwanza - Airport  
na Mwanza - Nyanguge**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM (K.n.y. MHE. MKIWA  
A. KIMWANGA)** aliuliza:-

Serikali ina mpango gani wa upanuzi wa Barabara ya Airport – Mwanza na Nyanguge – Mwanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara, imeanza kuboresha Barabara ya Mwanza – Nyanguge, sehemu ya Mwanza (Natta) – Buzuruga (km 4), kwa kupanua kuwa njia tatu urefu wa km 2. Bajeti ya jumla ya shilingi bilioni mbili zimetengwa katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo. Aidha, sambamba na upanuzi wa barabara hiyo, madaraja mawili yaliyoko eneo la Mabatini na Mlango Mmoja, yatapanuliwa na ujenzi wa kituo kimoja cha daladala pale Buzuruga, eneo ambalo lina msongamano mkubwa magari utafanyika.

Kazi zingine zinazoendelea kutekelezwa ili kupunguza msongamano wa magari katika sehemu ya Mwanza (Natta) - Buzuruga ni ujenzi wa daraja la juu la waenda kwa miguu eneo la Mabatini, kwa gharama ya shilingi bilioni moja. Mwaka ujao wa Fedha (2014/2015), tumepanga kuendelea na upanuzi wa km 2 zilizosalia hadi Buzuruga.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwanza – Airport, yenye urefu wa km 9, ina magari mengi hivyo inahitaji kupanuliwa na kuwa njia nne. Makisio ya gharama ya upanuzi wa Barabara hii ni shilingi bilioni kumi. Kutokana na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

ufinyu wa bajeti, Serikali itaangalia uwezekano wa kujenga barabara hiyo kadiri uwezo wa bajeti utakavyoruhusu.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupanua barabara ya kutoka Mwanza Mjini hadi Igoma ambayo imezidiwa na msongamano mkubwa wa magari na binadamu?

(ii) Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuziweka njia mbili mbili, yaani kutoka Mwanza Airport na kuelekea Mjini, barabara ambayo upana wake unatosha lakini wakati huu pamoja na watu waliolipwa barabarani ambao njia hii itaweza kutengenezwa vizuri, bado inaonekana msongamano umekuwa mkubwa kutokana na ukubwa wa kukua wa Jiji la Mwanza. Kuna mpango gani wa haraka kupanua njia kwenda njia mbili kutoka Mwanza Mjini hadi Airport na kurudi? Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba, Serikali tayari imeshaanza kulishughulikia suala la msongamano katika Jiji la Mwanza, kwanza, kwa kuweka taa za barabarani Mtaa wa Nyerere pamoja na Mtaa wa *Station Road* tumeshaweka taa za kuongoza magari. Pia kama nilivyosema, tunao mpango wa kujenga barabara ya kutoka Mwanza mpaka Airport ziwe njia nne; njia mbili kwenda na njia mbili kurudi. Tunaendelea na utaratibu huo na hizo barabara zingine kulingana na uwezo wa Serikali na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, mawazo yako Mheshimiwa ni mazuri na Serikali inayashughulikia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Desderius Mipata, atauliza swali hilo!

Na. 6

**Pori la Lwafi Game Reserve**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilitoa Pori la *Lwafi Game Reserve* kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori (*TANAPA*) kwa kuiomba *TANAPA* kurekebisha mipaka ya Pori hilo ili kutoa ardhi zaidi kwa Wananchi wanaopakana na Pori hilo ili kuondoa uhaba wa ardhi kwa Vijiji vya Mtapenda, China, King'ombe, Mlambo, Namausi, Msamba na Ng'undwe:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ombi la Wananchi wanaozunguka Pori hilo?

(b) Kwa kuwa Pori hilo lina Watumishi wachache sana kiasi cha kufanya kazi ya ulinzi kuwa ngumu sana; je, kuna mpango gani wa kuongeza Watumishi zaidi Mbuga ya Wanyama ya Lwafi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Lwafi lilikabidhiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi tarehe 10 Agosti, 2011 kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa wanyamapori. Pori la Lwafi lilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 284 lililochapishwa tarehe 24 Desemba, 1993 likiwa na eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,228. Aidha, Pori hili ni muhimu kuhifadhiwa kwa sababu ni chanzo cha Mito ya Lwafi, Ntemba na Kalambo, ambayo humwaga maji Ziwa Tanganyika na pia ni makazi ya wanyamapori adimu aina ya Sokwe.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

Mheshimiwa Spika, suala la kuomba kurekebishwa mipaka ya Pori la Akiba Lwafi, ndiyo tumelipata na ikiwa ni miaka miwili tu tangu tumekabidhiwa Pori hili. Ukweli ni kwamba, ipo haja kubwa ya kuongea na kuwaeleza Wananchi umuhimu wa kuhifadhi Pori hili na Mapori mengine kote nchini. Mwenendo mzima wa mabadiliko ya tabia nchi, ukame, majangwa, unatutaka tuwe makini sana katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua suala la upungufu wa Watumishi katika Pori la Akiba Lwafi na Mapori mengine hapa nchini. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara yangu imepewa kibali cha kuajiri jumla ya Wafanyakazi 459, wakiwemo Maafisa Wanyamapori 27 na Wahifadhi Wanyamapori, yaani Maaskari wa Wanyamapori 432, ambao wanatarajiwa kugawiwa katika Mapori mbalimbali nchini ikiwemo Pori la Akiba Lwafi ili kukabiliana na upungufu huu wa rasilimali watu hasa katika Mapori ya Akiba nchini kote.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ninayo maswali mawili ya Nyongeza.

(i) Vijiji vya King'ombe na Mlambo ni vya asili, inasemekana vipo ndani ya *Lwafi Game Reserve*. Licha ya Vijiji hivyo kuwepo hata kabla ya *Game Reserve* kuanza; je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu mkubwa wa kurekebisha mipaka hiyo ili kuepukana na migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na mahitaji ya ardhi ya kilimo kwa Wananchi?

(ii) Yapo Mapori mengi ya Akiba nchini likiwepo na Pori la *Uwanda Game Reserve*. Serikali haioneshi jitihada zozote za kuyaendeleza Mapori hayo, ikiwa ni pamoja na kuweka mipaka hadi kusababisha Wananchi kuingia, aidha, kwa kutokujua au kutokana na uhaba wa ardhi. Je, Serikali inao mpango gani mkakati wa kuendeleza Mapori hayo ikiwa ni pamoja na kuweka mipaka thabiti katika menea hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, Serikali inatambua kwamba, wakati mazungumzo yanafanyika na yanakamilika na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, mazungumzo haya kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na Serikali, kwa maana ya Wizara ya Maliasili na Utalii, yalikalika tarehe 10 Agosti, 2011 na Pori hili lote kama lilivyo, likakabidhiwa. Ninafikiri itakuwa ni muhimu na sisi kama Serikali tupo tayari kuendelea kufanya mazungumzo na Wananchi sehemu yoyote nchini ili tuweze kuhakikisha kuna uhifadhi endelevu. Uhifadhi ni lazima tushirikiane na Wananchi katika kuhakikisha mipaka inakuwa wazi.

Swali lake la pili, ni jinsi gani sisi kama Serikali tunaweka mipaka; tunao utaratibu kwanza wa kuongeza Watumishi katika suala zima la kusimamia Mapori haya kikamilifu. Vilevile Serikali inaendelea kuweka alama za kudumu katika mipaka ya Mapori kote nchini na tunafanya hili jambo kwa awamu.

Mwisho, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama kuna mambo ambayo anadhani ni lazima tuyaangalie, Serikali ipo tayari kuyasikiliza. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa migogoro iliyopo katika Mapori ya Akiba na Wananchi wanaoishi kandokando ni mikubwa na Mheshimiwa Naibu Waziri akiwa hapa Bungeni, alisema kwamba, ataunda Tume ya kuchunguza migogoro hii kupita katika maeneo ambayo yamepakana na Hifadhi, lakini mpaka leo hii taarifa hiyo haijatolewa!

Naibu Waziri alikuja Jimboni kwangu akakuta Wananchi wameonewa, ngo'ombe wao wamepigwa risasi, akaahidi kwamba Wizara ingeliweza kulipa ngo'ombe hao; leo hii ni karibu miaka miwili Wizara hii ikiwa inalalamikiwa kuingia mikataba kinyume cha sheria katika ...

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwanza, unasoma, halafu swali lenyewe ni refu!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, sisomi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, basi ninakuomba u-*summarize*.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Sisomi. Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara wamekuwa wakiingia mikataba kinyume cha Sheria katika mikoa iliyoko kandokando ya Hifadhi. Leo ni zaidi ya mwaka mmoja, Wilayani Meatu wameridhia mikataba ambayo ipo kinyume cha Sheria na tumewaomba kuja hawakuja.

Ninataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa nini Wizara yake inawahadaa Wananchi kwa kiasi hicho? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakuomba ujibu kwa kifupi. Ukipenda kujibu, jibu swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Luhaga Mpina, kama ifuatavyo:-

Ni kweli nilifanya ziara katika Pori la Maswa ikiwa ni sehemu ya ziara ambazo Wizara ya Maliasili na Utalii, tunazifanya nchi nzima. Tuliona matatizo makubwa sana ambayo Wananchi wa Maswa wanaokaa kandokando ya Pori la Akiba la Maswa wanakumbana nayo. Kimsingi, nimhakikishie Mheshimiwa Luhaga Mpina kuwa, Serikali imechukua hatua na inaendelea kuchukua hatua za kutatua hilo tatizo mara moja na lisitokee tena.

Tunafahamu kwamba, msongamano mkubwa wa watu ikiwa ni pamoja na *pressure* ya ng'ombe kuingia katika hili Pori la Akiba la Maswa limekuwa ni tatizo kubwa sana, ambalo tunaendelea kuzungumza na Wananchi wa eneo hilo, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, ilituhakikishia kwamba, mipaka ipo wazi, inaeleweka na inasimamiwa.

Niseme tu kwamba, Serikali kupitia ziara yangu, tuliahidi kulipa fidia ya ng'ombe ambao walikuwa wameuwawa ndani ya Pori la Akiba la Maswa na tulikubaliana mimi pamoja na Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwamba, hilo jambo litakuwa zuri kwa ajli ya mahusiano mazuri tu.

Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Luhaga Mpina kuwa, kama bado watekelezaji hawajafanya hivyo, ninafikiri kwanza wamenisikia; ni ahadi ambayo tutapenda itekelezwe mara moja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tatizo la migogoro ya mipaka kwenye mapori na maeneo ambayo yako karibu na maeneo oevu limekuwa kubwa; na kwa kuwa hivi karibuni kulikuwa na Operesheni Tokomeza, ambayo ilipelekea vijiji vingi kuunguzwa ikiwemo Kitongoji cha Mchangani kilichopo katika Jimbo la Momba ambacho kilipewa Nambari ya Usajili na Mamlaka ya *TANAPA* wanayo (TZB 00032); lakini Serikali ilienda kukichoma Kijiji hicho chote na mpaka sasa Wananchi wanateseka.

Sasa tunataka *TANAPA* watuambie ni namna gani wanaweza kuwasaidia watu wale na kwenda kuwaainishia mipaka ili kuondoa mgogoro ambao unaweza kujitokeza mara nyingine? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali imesema na hapa ninarudia tena kwamba, Operesheni Tokomeza, ambayo lengo lake ni kuokoa maisha na uwepo wa wanyamapori Tanzania,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

pamoja na kwamba imesitishwa kwa muda, kwa njia moja ama nyingine, kasoro ambazo zilijitokeza, zitakaporekebishwa itaendelea.

Pili, kwa sababu tumepokea malalamiko mengi kwa Wananchi na kutoka pia kwa Waheshimiwa Wabunge, kuwa baadhi ya kasoro zilijitokeza wakati wa zoezi hili la Operesheni Tokomeza. Tume Maalum ambayo umeanzisha ikiongozwa na Kamati husika ya Bunge, inaendelea kufanya kazi nchi nzima na tunaamini kwamba, zile kasoro ambazo zilijitokeza za utendaji ni lazima zirekebishwe.

Operesheni hizi zinatakiwa ziwe salama, zinatakiwa zisiumize Wananchi na vilevile zisifanye uharibifu ambao hauna sababu. Ni muhimu sana tukaangalia ni nini kilitokea kila mahali nchini na Wananchi wawe tayari kushirikiana na Tume hiyo ya Bunge ili tuweze kupata taarifa ambayo itatusaidia kufanya maamuzi ambayo tunapoendelea na Operesheni ya Kuokoa Wanyamapori, tutakuwa tunafanya hivyo kwa kuzingatia haki za binadamu na usalama wa raia na mali zao.

**SPIKA:** Waheshiwa Wabunge, tupo nyuma ya muda, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 7

### **Kukomesha Uvunaji Haramu wa Mbao Ndani ya Misitu**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI (K.n.y. MHE. FAITH M. MITAMBO)** aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi la uvunaji haramu wa mbao ndani ya Misitu ya Hifadhi Wilayani Liwale licha ya juhudi za Serikali kukomesha uvunaji huo:-

(a) Je, kwa nini uvunaji huu haramu unaendelea kwa kasi badala ya kupungua?

(b) Je, Serikali imejipangaje kukomesha tatizo hili?



**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uvunaji haramu wa mazao ya misitu katika Wilaya ya Liwale, unasababishwa na mambo mbengi, ikiwa ni pamoja na misitu kuwa chanzo rahisi cha kupata riziki, ongezeko la shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na makazi, utegemezi mkubwa wa misitu kama chanzo kikuu cha nishati, uhaba wa Watumishi walioajiriwa ikilinganishwa na eneo la misitu analolisimamia na kubwa zaidi ni watu kutokujali na kuheshimu sheria zilizopo. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Novemba, 2013 Serikali imefanikiwa kukamata jumla ya mbao 11,008 zilizovunwa kinyume cha sheria katika Wilaya ya Liwale na watuhumiwa wawili kesi zao zipo mahakamani na zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Wizara yangu imejipanga kukomesha tatizo la uvunaji haramu wa misitu kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Wakala wa Misitu (*TSF*), umeanzisha mchakato wa Usimamizi Shirikishi kwenye misitu ambayo hajahifadhiwa kisheria Wilayani Liwale ili iwe na usimamizi shirikishi hususan kwenye Misitu ya Angai na Barikiwa ambako Wananchi watashirikishwa kuilinda misitu hiyo.

(ii) Kutoa elimu kwa njia ya mikutano na semina wakati wa shughuli za ugani katika ngazi za Vijiji, Wilaya Mikoa na Taifa kwa ujumla.

(iii) Kuweka maboya na mabango ya kutambulisha maeneo ya misitu (hii ni mipaka). Kuhakiki mipaka na kubaini mianya iliyopo ya uvunaji holela na ukwepaji kulipa ushuru wa mazao ya misitu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

(iv) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa kushtukiza, kuhakiki nyaraka katika Ofisi za Maafisa wa Misitu wa Wilaya, Maafisa wa Vituo vya Ukaguzi na maeneo ya uvunaji.

(v) Imeanzisha kanda saba ili kuimarisha usimamizi wa rasilimalli za misitu na nyuki nchini kote.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninataka niseme ya kwamba, mimi mwenyewe nimetembea kuanzia Kilwa kupitia huo Msitu kwenda Liwale mpaka Nachingwea. Kwa kweli inasikitisha sana kuona miti ile mikubwa ambayo ilizaa miaka na miaka imelala chini imekatwa kwa siku mbili au siku tatu.

Pamoja na jitihada za Serikali za kufanya semina za kuweka mchakato wa usimamizi shirikishi, ukaguzi wa mara kwa mara na uwekaji wa kanda, lakini hali ni mbaya. Tunataka na tunaiomba Serikali ichukue jitihada za haraka sana kwenda kuangalia hali ilivyo kule Liwale, Kilwa na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Fatma Mikidadi, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninaomba kwa niaba ya Wizara na Serikali, tumpongeze na tumshukuru sana kwa ufuatiliaji wake kwa hili jambo ambalo ni kubwa. Eneo analolitaja kuanzia pale Kilwa mpaka Nachingwea, sisi kama Serikali tunakiri kwamba, hali ni mbaya na misitu inazidi kutoweka.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

Nataka niseme kuwa, mwezi Desemba, 2012, tulifanya zoezi la *Task Force*, tukishirikiana na *TSF* na tuliwashtukizia tukakamata mbao zaidi ya 4,225. Zoezi lingine lilifanywa na Halmashauri, walikamata mbao zaidi ya 1,980.

Labda mfano wa mwisho tu, katika Operesheni inayoendelea ya Tokomeza, mpaka sasa hivi katika hii Wilaya peke yake, tumekamata mbao haramu zaidi ya 1,883. Ukweli ni kwamba, hali ya misitu ikiachwa ikaendelea kama ilivyo, misitu itaisha na hasa misitu ya asili. Tunajipanga upya na ninaomba Waheshimiwa Wabunge, wote tushirikiane ili tuweze kuokoa janga hili ambalo linaendelea.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na wimbi la mbao kutoka nchi jirani ya Msumbiji kuletwa Tanzania. Hali hiyo imejitokeza katika Wilaya ya Masasi na Wilaya yetu ya Tunduru.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia zoezi hilo lisije likaleti mahusiano mabaya kati ya nchi yetu na majirani zetu wa Msumbiji?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunao utaratibu katika Nchi za *SADC* kama ulivyo katika Nchi za Afrika ya Mashariki wa kuwa na biashara huria. Mazao yanayotokana na mbao tunayahitaji katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kitu ambacho tunasema, moja; mazao haya lazima yasiwe mazao haramu, yavunwe kwa utaratibu uliokubalika kitaalam na yavunwe kwa kulipa kodi mbalimbali za Serikali.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

Tukitambua kwamba, kuna mbao zinazotoka katika nchi jirani ya Msumbiji, huwa kuna namna ya *point of origin* ambako tunaweza tukazitambua hizi mbao zimetoka kule, zimethibitishwa na kulipiwa kodi za Serikali mpaka zinakoenda.

La mwisho, ningelipeda niseme kwamba, kuna watu ambao wanakata mapori yetu katika maeneo ya mipaka, halafu wanasema hizo mbao zimetoka nchi jirani. Ninaomba kwanza, niwaonye waache mara moja, kwa sababu adhabu tunayowachukulia ni kubwa. Wengi tumewakamata na tutaendelea kufanya hivyo tuhakikishe tunaokoa mapori haya ambayo yanapotea.

Ninamwomba sana Mheshimiwa Mtutura, ikiwa ni pamoja na Wabunge wengine kama nilivyosema, tuendeleo kushirikiana na tutashirikiana na wewe na wenzako ili tuhakikishe tunawatambua hao ambao wanakuwa ni kero katika ulinzi shirikishi wa maliasili zetu. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Pamoja na kwamba, tatizo la misitu limekuwa kubwa na uvunaji wake umekuwa mkubwa, takwimu zinaonesha kwamba, kuanzia sasa mpaka miaka saba misitu itakuwa imeisha Tanzania. Hizi ni takwimu zinazoonesha kwenye masuala ya mkaa bila mbao.

Mheshimiwa Spika, toka Bunge hili la Kumi limeanza, ushauri mkubwa umetolewa na Wabunge pamoja Hotuba za Kambi za Upinzani juu ya tatizo hili. Nilitaka kujua Wizara mpaka sasa imepunguza tatizo hili kwa kiwango gani ili tuokoe misitu yetu, yaani kwa maana kwamba, mmepunguzaje hii *sustainability* kwa miaka saba mpaka kumi ambapo misitu itakuwa imekwisha. Wizara imefanya nini ili kutuepusha katika tatizo hilo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba ujibu kwa kifupi sana, muda umetukalia vibaya.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu swali moja fupi la Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, kama ifuatavyo:-

Hali ambayo inaendelea ya misitu Tanzania ni tatizo kubwa, kwa sababu misitu mingi sana inakatwa, ndiyo maana Serikali kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tunajitahidi tuhakikishe kwamba, tunaweka *sustainable modal* ambayo itatusaidia sisi kuanza kupanda misitu upya, kuhifadhi misitu ambayo inaendelea ile ya asili kwa njia shirikishi na tunaanzisha mikakati mingine ambayo itawahusisha Wananchi na jamii mbalimbali binafsi waweze kushiriki katika kumiliki baadhi ya misitu.

Hata hivyo, ningelipenda niseme kwamba, Tanzania sasa hivi tuna *Forest Ranger* mmoja; hawa ni Wasimamizi wa Misitu, anasimamia zaidi ya hekta 22,000, wakati *standard* ya kawaida, *Forest Ranger* mmoja anapaswa kusimamia hekta zisizopungua 5,000. Tatizo la rasilimali watu ni kubwa.

Serikali inaendelea kujipanga ili tuweze kukabiliana nalo na kama nilivyosema, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote, tushirikiane katika kuhakikisha wale ambao wanachoma moto misitu kwa kuihujumu nchi, tunawakamata na tunawapeleka katika vyombo vya sheria kwa kutumia utaratibu ambao upo wazi na unaozingatia Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tupo nyuma sana na sasa naomba tuendelee na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya atauliza swali hilo.

Na. 8

### **Kuwezesha Wavuvi wa Ziwa Tanganyika**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi katika kuimarisha uvuvi katika Ziwa Tanganyika?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi, imeandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi ya mwaka 2012/2013 – 2016/2017 ambayo imeainisha maeneo ya utekelezaji yanayolenga kuwa na uvuvi wenye tija. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilmali za uvuvi, kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo na masoko, kutoa elimu ya uvuvi endelevu, ukuzaji viumbe kwenye maji, matumizi ya teknolojia sahihi za uhifadhi wa mazao ya uvuvi mifugo na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeanzisha mfumo wa kutoa ruzuku kwa wavuvi wadogo kama ilivyo katika Sekta za Mifugo na Kilimo utakaotolewa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. NAIBU WAZIRI  
WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI)]

kwa utaratibu wa Mfuko wa Mzunguko, yaani *Revolving Fund*. Jumla ya Shilingi bilioni 1.9 zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi wadogo kupata vyombo na zana za uvuvi ili waweze kufanya uvuvi wenye tija na endelevu. Ruzuku hiyo itatumika kununua Boti za Uvuvi na viambata vyake, yaani injini, kasia, kamba na vinginevyo; na zana za uvuvi, yaani nyavu za uvuvi na ndoano. Chini ya utaratibu huu, maboti 50 na viambata vyake na zana za uvuvi zipatazo 15,562 zinatazamiwa kununuliwa.

Ruzuku hii itatolewa kwa wavuvi wakiwemo wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Waombaji wa ruzuku watapitisha maombi yao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya husika kwa ajili ya kupitiwa na kuona kama yanakidhi vigezo kabla hayajawasilishwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi Shirikishi wa Kikanda wa Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (*PRODAP*) unaotekelezwa kuanzia mwaka 2008 hadi Desemba mwaka 2013, mialo minne ya kupokelea Samaki ya Kibirizi (Kigoma Ujiji), Muyobozi (Kigoma), Ikola (Mpanda) na Kirando (Nkasi) imejengwa. Aidha, chanja za mfano za kuanika dagaa kwenye mialo zitawekwa na wavuvi wapatao 3,713 watanufaika. Vilevile, jumla ya vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (*BMUs*) 20 katika Halmashauri za Kigoma, Vijiji tisa, Kigoma Ujiji viwili, Mpanda Vijiji vitano na Nkasi vinne vimeanzishwa na kupewa mafunzo ya uvuvi endelevu.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mhonga, swali la nyongeza.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hali ya uvuvi ni duni na ni masikini sana. Sasa napenda kusesitiza kwamba elimu itolewe vya kutosha ili wajue ni vigezo gani vinavyohitajika.

Sasa naomba kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

Ruzuku iliyotolewa katika Sekta ya Kilimo imeonekana kuna matatizo mengi sana na ufisadi mkubwa. Je, Serikali imejiandaaje kuhakikisha kwamba ruzuku itakayotolewa kwa wavuvi haitakuwa na matatizo kama yaliyotokea katika Sekta ya Kilimo?

Pili, nataka kujua; kwa kuwa, Shilingi bilioni 1.9 iliyotolewa ni kwa ajili ya Ziwa lote la Tanganyika: Je, wavuvi wa Mkoa wa Kigoma watapata kiasi gani katika ruzuku hii iliyotengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):** Mheshimiwa Spika, ruzuku hii itatolewa kwa utaratibu ambao sasa umebuniwa kama vile ilivyo katika Kilimo na Ufugaji.

Kwa hiyo, yale mabaya yote yaliyokuwa yamejitokeza katika utoaji wa ruzuku kwenye kilimo na ufugaji yatazingatiwa wakati wa utoaji wa ruzuku hii. Ndiyo maana nimesema kwamba maombi yote yatapitishwa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, yataangaliwa kuona wale wavuvi wanaoomba wanakidhi vigezo kwa kiasi gani na baadaye ndiyo yatawasilishwa Wizarani na ruzuku kutolewa.

Kuhusu wavuvi wa Mkoa wa Kigoma watanufaika kwa kiasi gani katika bajeti iliyotengwa? Hii yote itategemea na wavuvi wenyewe watakavyochangamka kupeleka hayo maombi na kukidhi vigezo ambavyo vimewekwa, kwa sababu kwa sasa haijatengwa kwamba Shilingi kadhaa ni za Mkoa fulani na kiasi kadhaa ni cha Mkoa fulani, isipokuwa ni kutegemeana na maombi yatakayowasilishwa ndivyo wavuvi wa Mkoa huo watakavyoweza kunufaika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Ramo Makani



**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, uchumi wa Taifa utaimarika tu pale ambapo tutaimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja, na kwa kuwa Sekta ndogo ya Uvuvi ni sehemu ya sekta kubwa ya kilimo kwa ujumla wake chini ya Mkakati wa Taifa wa Kilimo Kwanza; na baada ya kusikiliza majibu ya swali la msingi ambalo lilikuwa sana sana linazungumzia uvuvi katika maziwa, nimevitika kuuliza swali kuhusiana na wavuvi katika ukanda wa Pwani.

Je, majibu yaliyotolewa na Serikali kwa upande wa uvuvi katika maziwa unawahusu pia wavuvi wadogo wadogo katika maeneo ya ukanda wa Pwani au kama kuna mikakati mingine tofauti, basi napenda kusikia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi majibu, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa kila ziwa na ukanda wa bahari pia, mpango wa kuwezesha wavuvi upo. Kwa upande wa Ukanda wa Pwani Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani, yaani *Marine and Coast Environment Management Project* unaotekelezwa kuanzia mwaka 2005 mpaka mwaka 2012, wavuvi 4,000 waliwezesha katika miradi ya uvuvi 240 yenye thamani ya Shilingi karibia bilioni nne.

Kwa hiyo, hata katika utaratibu huu, nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba wavuvi wote nchini wadogo wadogo watapitisha tu maombi yao katika Halmashauri husika na kama watakuwa wanakidhi viwango, hajjalishi kwamba wanavua Pwani au katika maziwa na wao pia watashiriki katika ruzuku hii.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendeleo na swali linalofuata kwa Wizara ya Maji. Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee atauliza swali hilo.

Na. 9

**Kupungua kwa Kina cha Maji Ziwa Victoria**

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR (K.n.y. MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE)** aliuliza:-

Ilibainika kuwa maji ya Ziwa Victoria yalikuwa yanapungua kina kiasi cha kufanya Meli kushindwa kuegeshwa Bandarini:-

- (a) Je, Serikali inaweza kueleza sababu ya hali hiyo?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupungua kwa kina cha maji ya Ziwa Victoria kulionekana kwa kiwango kikubwa kati ya miaka ya 2006/2007 ambapo kina cha maji kilishuka kwa takribani mita mbili. Baada ya utafiti wa kina uliofanywa na *Lake Victoria Environment Management Project (LVEMP)* pamoja na wadau wengine, ilibainika kuwa mitambo mipya ya kufua umeme kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria iliyojengwa huko Uganda kwenye eneo la Jinja ilikuwa inatumia maji mengi zaidi kuliko inavyokubalika. Pia, mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotegemea moja kwa moja maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kila siku kulichangia kupungua kwa kina cha Ziwa hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua kubwa iliyochukuliwa hadi sasa ni kuundwa kwa Sera ya kusimamia matumizi ya maji ya Ziwa Victoria chini ya usimamizi wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MAJI]*

Sekretarieti ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ya mwaka 2012. Sera inalenga kuunda mkakati wa pamoja wa kufuatilia maji yanayotoka kwenye Ziwa Victoria kupitia Mto *Nile* na kuelekeza Bahari ya *Mediterranean* na kwingineko na pia kusimamia kwa pamoja uchepushaji wa maji ya Ziwa Victoria katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utekelezaji wa Sera hiyo umeshaanza chini ya utaratibu wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (*LVBC*).

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nassib, swali la nyongeza.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mkakati mkubwa wa kutumia maji ya *Lake Victoria* kwa ajili ya binadamu hasa kwa maeneo ambayo yanazunguka ziwa hili. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba matumizi haya makubwa ya maji yatasababisha kupungua kwa kina cha maji katika *Lake Victoria*?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina mipango ya kuwapatia wananchi wanaoishi ukanda wa Ziwa Victoria kupata maji ya Ziwa Victoria badala ya kuwaacha wahangaike na maji ya visima ambayo hayana uhakika.

Mkakati mmojawapo ni kutoa maji kutoa Ziwa Victoria kuyapeleka Igunga, Nzega na Tabora na mkakati wa pili ni kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Magu, Misungwi na Lamadi na wa tatu ni kuyapeleka katika Miji ya Bariadi, Lagangabilili, Mwandoya, Meatu, Maswa na Kishapu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiwango cha maji yanayotumiwa na binadamu ni kidogo sana, hakiwezi kuathiri matumizi ambayo yanaongelewa katika *case* hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba haina madhara yoyote bali ni kiwango kidogo sana ambacho binadamu anatumia.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mojawapo ya sababu zinazosababisha kupungua kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria ni shughuli za kibinadamu katika maeneo oevu ambayo hukamata maji kwa ajili ya kujaza katika Ziwa hilo.

Nataka kujua, kwa nini Serikali haichukui jitihada za kuwasaidia wananchi wa maeneo oevu ili kusudi waweze kuendesha shughuli zao bila kuathiri ukamataji wa maji na ulishaji wa maji hususan katika sehemu za Lutoro, Ngenge na sehemu zote za Mto Ngono ili kusudi maji yaweze kwenda vizuri lakini baada ya Serikali kuwasaidia?

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, upo mpango unaosimamiwa na *Lake Victoria Environmental Management Project (LVEMP)* ambao kazi yake ni kuanzisha miradi mbalimbali mbadala ambayo itawafanya wananchi ambao wanafanya shughuli kando kando ya Ziwa Victoria zinazoathiri yale maji waachane na zile shughuli na badala yake wafanye shughuli nyingine zitakazowaongezea kipato zaidi ya kile ambacho wanakipata sasa hivi. Kwa mfano, tuna miradi katika maeneo uliyosema kama ya ufugaji wa nyuki. Kwa hiyo, inawaondoa wananchi kwenye shughuli zinazotegemea ziwa, badala yake kupata kipato kwa kutumia miradi kama hiyo ya nyuki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Arfi, swali la nyongeza.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Ziwa Victoria lina mpango mkakati wa kuweza kulinusuru, Serikali ina mpango mkakati gani wa kulinusuru Ziwa Rukwa ambalo linakauka kwa kasi zaidi?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, maziwa yote yanaathirika na mkakati ambao nimeusema unakwenda kwenye maziwa yote na kila ziwa lina jumuiya zake ambazo zinasimamia ikiwemo Ziwa Rukwa ambalo lipo katika Mkoa wa Rukwa.

Nataka nimhakikishie kwamba mikakati ipo na tunaweza tukampa *details* za undani wake nini kinafanyika ili aweze kufahamu zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na swali linalofuata, Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Khatib Said Haji.

Na. 10

### **Ukadiriaji wa Bei ya Magari yanayotumika**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Yapo malalamiko makubwa juu ya utaratibu wa TRA wa ukadiriaji wa bei ya magari yaliyotumika kutoka nje ya nchi:-

- (a) Je, *TRA* inatumia utaratibu gani ambao ni sahihi katika kuthibitisha thamani halisi ya gari husika lilivyonunuliwa na kutozwa kodi stahiki na halali?
- (b) Je, *TRA* haioni kuwa inafanya kitendo cha dhuluma kuweka bei elekezi kwa magari hayo kwa kuzingatia kigezo tu cha mwaka lilipotengenezwa?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kuona kuwa baadhi ya walipa kodi wengi wanaitumia vibaya fursa ya kutozwa ushuru wa magari kwa kuangalia bei ya gari iliyoidhinishwa na nyaraka za mnunuzi, yaani *invoice*, kwa kubaini kuwa nyaraka nyingi siyo halisia na zinatengenezwa na muuzaji kwa makubaliano na mnunuzi ili zimsaidie kulipa kodi kidogo zaidi; Serikali ilianzisha utaratibu mpya wa kutambua bei halisi za magari itakayotumika kumtoa kodi mwagizaji gari nje ya nchi.

Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato imekuwa ikishirikiana na mawakala wa Kampuni za kutengeneza magari, kama *Toyota (T) Ltd, CMC* na wengineo katika kupata bei halisi ya magari mbalimbali katika masoko tofauti ya magari duniani. Pia, Mamlaka ya Mapato inatumia mitandao (*internets*) ya masoko tofauti ya magari ya Japan ambao nao wanazipata kutoka kwa Mawakala wa magari wa nchi hizo (*Car Dealers Networks*). Bei hizo huchambuliwa na kuingizwa katika orodha yetu ya bei za magari (*Price Database*) na kutumika kutathmini na kukadiria bei stahiki ya magari yanayoingia nchini ambayo hutumika katika msingi wa kutoza ushuru wa magari.

(b) Mheshimiwa Spika, bei elekezi inayowekwa kwa magari yaagizwayo nje ya nchi haipangwi kwa kuangalia mwaka ilipotengenezwa tu. Pamoja na kuangalia mwaka ilipotengenezwa gari na bei yake mwaka huo huangaliwa pia vigezo vingine kadhaa kama aina au muundo (*Model*) wa gari, mtengenezaji na ukubwa wa injini (*CC*). Yote haya yanachukuliwa pamoja na kutilia maanani uchakavu (*depreciation*) wa gari na hali hii ndiyo hutupatia bei elekezi ambayo Serikali hutumia kutoza ushuru stahiki kwa kila gari.

Kwa hiyo, siyo kitendo cha dhuluma, bali ni utaratibu unaozingatia vigezo vingi ambavyo pia hufuatwa na nchi nyingine duniani. Ahsante!

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khatibu Said Haji, swali la nyongeza.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, Serikali iliondoa utaratibu wa kuzitambua nyaraka halisi za waletaji magari kwa dhana kwamba wanashusha thamani; lakini Watanzania wengi wanaleta magari yaliyotumika ambayo hununuliwa mnadani na bei za mnadani zinabadilika muda wowote. Je, Serikali haioni kutumia vigezo vingine vyovyote ukiacha bei halisi ya mnunuzi ambayo amenunua ni utaratibu ambao bado unaonekana ni kuwadhulumu wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Watanzania wengi wananunua magari kutoka nchi za Japan, Dubai na Uingereza na katika nchi hizo *TBS* wanakagua magari hayo kuthibitisha ubora wa viwango vyake: Je, Serikali haioni umuhimu wa Serikali kuitumia *TBS* hiyo hiyo kuthibitisha uhalisia wa bei wanazonunua Watanzania ili kuondokana na kero wanayoipata ya magari yao kuishia kufilisiwa mnadani inapofika Bandari ya Dar es Salaam? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuwa magari mengi hununuliwa mnadani, hiyo pia imezingatiwa na *TRA* wakati wanapopanga bei elekezi kwa kuangalia *Car Dealers Networks* na wauzaji mbalimbali wa magari kutoka nje. Kwa hiyo, hilo pia limezingatiwa na kuangalia hali halisi ya bei ambayo magari yanauziwa katika minada hiyo ya nje.

Kuhusiana na swali pili kuwa *TBS* itumiwe nayo vilevile kuthibitisha bei, hili ni jambo ambalo linaweza likazungumzwa. Lakini hata hivyo bado bei ambayo *TRA* wanaipanga inaangalia *invoice* ambayo inaletwa na mnunuzi wa gari lakini na vigezo vingine vyote ambavyo nilivitaja katika jibu langu la msingi. Lakini siyo suala baya kuangalia kama *TBS* wanaweza pia wakathibitisha bei hizo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na mwuliza swali la msingi. Ukweli ni kwamba pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini bado wananchi wanalalamika kutokana na namna ambavyo *TRA* imekuwa ikikadiria hizo kodi kutokana na manunuzi ambayo mtu husika anakuwa amefanya.

Mheshimiwa Spika, limeongelewa suala la kwenye minada ama kunakuwa na *promotions* watu wananunua vifaa kule na kuvileta hapa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kubadilisha huo utaratibu na ama ifanye utafiti igundue ni wafanyabiashara wangapi ambao labda wamekuwa ni wadanganyifu kutokana na zile bei ambazo wanakuwa wananunua kule ili waweze kumwachia mnunuzi kwa gharama ile aliyonunua kule alikotoka? Kwa mfano, wanunuzi wanaotoa vifaa China mara nyingi wanakwenda wakati wa *Promotion*, vifaa vile vinauzwa kwa bei nafuu, lakini wanapofika bandarini *TRA* wanawaongezea bei. Bado hiyo ni kumdhulumu mwananchi Mheshimiwa Waziri!

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli inawezekana kuna wakati ambao wananchi wanaleta *invoice* ambazo ni sahihi. Lakini Waheshimiwa Wabunge tunafahamu kuwa watu wengi wanaleta *invoice* mbili mbili. Mimi binafsi nimeshanunua gari na nikaulizwa kama nataka *invoice* ndogo au unataka *invoice* halisi?

Kwa hiyo, ni kawaida, tunaulizwa. Wapo watu wanafanya udanganyifu. Kwa hiyo, tujitahidi, uaminifu ni muhimu. *TRA* nao vilevile watajitahidi kuangalia jinsi gani ya kuboresha. Lakini udanganyifu Waheshimiwa Wabunge upo katika mambo mengi tu.



## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa watu wengi hawapendi kulipa kodi, ni kawaida. Kwa hiyo, tusikatae kuwa watu hawadanganyi. Lakini vilevile tukumbuke kuwa lazima na sisi tupate kodi stahiki ili tuweze kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, naomba tusaidiane. Mapendekezo yote tutayachukua tutafanyia kazi, tutafanyia utafiti zaidi, kwa sababu utafiti umeshafanywa ndiyo ikagundulika kwamba kuna udanganyifu, lakini tutajitahidi. Wadanganyifu ni wengi kuliko tunavyoweza kufikiria. Lakini tutajitahidi, lakini vilevile na wananchi nawaasa na wenyewe pia wajitahidi kuwa wakweli ili hili tatizo ambalo mwisho wake ni kutokuaminiana liishe. Kwa hiyo, nafikiri kwa kifupi naweza kujibu hivyo kwa sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos, kwa niaba yake Mheshimiwa Zungu.

Na. 11

### **Kupanua Wigo wa Kodi Kukusanya Mapato kwa Wingi**

**MHE. MUSSA Z. AZZAN (K.n.y. MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO)** aliuliza:-

Mara nyingi Serikali imekuwa ikishauriwa kupanua wigo wa kodi ili kukusanya mapato kwa wingi zaidi:-

(a) Je, ni kodi gani mpya zimependekezwa kwa mwaka huu wa fedha?

(b) Je, ni kiasi gani cha mapato ya ziada kimetolewa kukusanywa?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato:-

(1) Kuanzisha kodi ya Sh. 50/= kwa lita kwenye mafuta ya petrol na dizeli kwa ajili ya kugharamia kusambaza umeme vijijini;

(2) Kuanzisha kodi ya zuio ya 5% kwenye huduma za ushauri, yaani (*consultants*);

(3) Kuongeza bidhaa kwenye orodha ya bidhaa zinazotowza ushuru wa bidhaa na kuzitoza ushuru wa bidhaa (*excise duty*);

(4) Kutoza ushuru wa bidhaa wa 14.5% kwenye huduma zote za simu za mkononi badala ya muda wa maongezi peke yake. Katika ushuru huo 2.5% zitatumika kwa ajili ya kuwekeza katika Sekta ya Elimu; na

(5) Kuanzisha ushuru wa bidhaa kwa kadi za simu (*sim card*) kwa wamiliki wa simu za mkononi kwa kiwango cha Sh. 1,000/= kwa kadi ya simu kwa kila mwezi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika robo ya kwanza ya fedha 2013/2014 hatua zilizochukuliwa za kupanua wigo wa kodi zilitarajiwa kuiletea Serikali mapato mapya ya Shilingi bilioni 290,526.4. Makusanyo halisi hata hivyo yalikuwa ni asilimia 81 tu ya lengo, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na kutokutekelezwa kwa hatua mbili, yaani kutoza ushuru wa bidhaa katika huduma za uhawilisho wa fedha na ushuru wa bidhaa wa utumiaji wa kadi za simu (*sim card tax*). Hatua hizi zilitarajiwa kuchangia Shilingi bilioni 82,103.5. Katika robo ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

kwanza ya mwaka hazikuweza kutekelezwa kutokana na kufunguliwa kwa kesi za kupinga utozwaji huo katika Baraza la Rufaa za Kodi, Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama Kuu.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zungu, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri: Je, atakubali kwamba kwa namna alivyozungumza sasa hivi kwamba watu wengi wanadanganya kwa kutokulipa kodi kutokana na kodi zenyewe kuwa kubwa mno ukilinganisha na nchi nyingi sana?

Swali la langu la kwanza ni kwamba *excise duty* sasa hivi inawafanya Watanzania wengi kushindwa kunywa soda wala maji baridi kutokana na *excise duty* kuwa kubwa? Wangeweza kupunguza *excise duty* wangepata fedha nyingi sana kutokana na watu wengi kunywa soda hizi na maji baridi.

La pili; Je, Serikali ina mpango wowote sasa hivi ku-*map* wafanyabiashara na kuwapunguzia wafanyabiashara wadogo kwenye suala la *VAT* ili *compliance* ya ulipaji kodi iwe kubwa na Serikali ipate mapato makubwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, tunapokea pendekezo la kupunguza *excise duty* kama njia mojawapo ya kufanya watu wengi zaidi walipe kodi. Lakini kama mnavyofahamu, hizi kodi tayari zimeshapitishwa, *Finance Bill* ilishapita, ilipitishwa katika Bunge hili. Kwa hiyo, kama ni mapendekezo itabidi yaje yafanyiwe utaratibu baadaye tutakapoangalia uwezekano ama la.

Kuhusiana kupunguza *VAT* kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo, sasa hivi tunategemea kuleta Bungeni Muswada wa *VAT*. Sasa naamini katika huo Muswada tunaweza tukatoa mapendekezo jinsi gani hizo *VAT*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

ziwe zinatozwa ili kila mtu aweze ku-*comply* kwa urahisi zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika utekelezaji wa Kodi ya Ushuru kwa bidhaa ya kodi za simu kwa wamiliki wa simu za mkononi ulileta mkanganyiko mkubwa sana kwa wananchi kutoelewa: Je, Serikali imechukua hatua gani kuondoa mkanganyiko huo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kodi ya simu *card* ilileta mkanganyiko ambao ulitokana na aidha na watu kutokuelewa vizuri hiyo kodi itatozwa vipi au tu kuona kuwa ni kodi ambayo labda ilikuwa ni kubwa sana kwa watumiaji wengi wa simu. Kwa sasa hivi siwezi kuzungumzia sana juu ya suala hili kwa sababu limeshapelekwa Mahakamani kupingwa. Lakini kwa kifupi hii ni kodi ambayo Serikali iliona inafaa na inawezekana kulipika kwa watumiaji wengi wa simu. Kwa sababu imeonesha kabisa kuwa mitandao ya simu inatozwa hela zaidi ya hiyo Sh. 1,000/= kwa wananchi hata bila ya wao wenyewe kuwa na taarifa wala kutoa vibali.

Kwa hiyo, tukaona kwamba hili ni jambo ambalo linawezekana na ndiyo maana Serikali lililipitisha hapa Bungeni ili itumike. Lakini kwa sasa hivi itabidi tungoje Mahakama itakavyoamua ndiyo itajulikana hatma yake.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Sheria na Katiba. Mheshimiwa Michael Laizer. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Anne Kilango.

Na. 12

## **Huduma ya Mahakama ya Longido**

**MHE. ANNE K. MALECELA (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Wilaya ya Longido haina Mahakama ya Mwanzo wala Mahakama ya Wilaya:-

Je, Serikali itajenga lini Mahakama ya Mwanzo na ya Wilaya Longido?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Mahakama Wilayani Longido na imetenga fedha katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2013/2014 kwa kuanza na ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Longido ili kusogeza huduma za Mahakama kwa wananchi wa Longido. Aidha, Serikali itahakikisha kwamba Mahakama ya Wilaya ya Longido inajengwa kwa siku za baadaye kulingana na bajeti itakavyoruhusu.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo nimeyaelewa, naomba kuuliza swali la nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kuwahakikishia vipi wananchi wa Wilaya ya Longido kuhusu hii Mahakama ya Mwanzo kwamba itajengwa katika *speed* ambayo itaweza kuwaondolea kero waliyonayo sasa hivi?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba Mahakama dhamira yake kuu ni kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Tunatambua adha ambayo wananchi wa Longido wanaipata. Hivi sasa wanazo Mahakama za Mwanzo mbili tu; Mahakama ya Mwanzo ya Namanga na Mahakama ya Longido Mjini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kupitia kwako, napenda nimpongeze Mheshimiwa Lekule Laizer, hivi sasa shughuli za Mahakama ya Wilaya pamoja na shughuli ya Mahakama ya Mwanzoni zinafanyikia katika Ofisi ya Mheshimiwa Mbunge. Tunalitambua hilo, tutalipa uharaka sana na tunajitahidi katika mwaka huu wa fedha kabla haujaisha Mahakama hiyo ya Mwanzo itakuwa imejengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea. Hii ilikuwa Longido; kwa hiyo, hakuna Longido mbili.

Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, kwa niaba yake, Mheshimiwa Njwayo.

Na. 13

**Mahakama ya Mwanzo Kata ya  
Nanyumbu Kukosa Hakimu**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. DUNSTAN D. MKAPA)** aliuliza:-

Ingawa jengo la Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Nanyumbu lilikarabatiwa miaka kadhaa iliyopita, lakini sasa jengo hilo limechakaa tena kwa sababu halitumiki kabisa kutokana na kukosa Hakimu:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Hakimu katika Mahakama hiyo?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Mkapu, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli jengo la Mahakama ya Mwanzo Nanyumbu lilikarabatiwa muda mrefu uliopita na hivi sasa limechakaa sana.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mahakama ya Tanzania, Serikali inalifahamu tatizo la kuchakaa kwa jengo hili na mengine mengi nchini na inao mpango wa kukarabati majengo haya kwa awamu kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na lini Serikali itapeleka Hakimku katika Mahakama hiyo ya Mwanzo Nanyumbu, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Mahakama husika imeshapatiwa Hakimku Mkazi mmoja kuwezesha Mahakama hiyo kutumika.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Njwayo, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na jambo jema la kuwapelekea wananchi Hakimku Mkazi wa Mahakama ya Mwanzo pale Nanyumbu, naomba nimwulize swali moja Mheshimiwa Naibu Waziri na lenyewe ni kwamba: Wananchi wa Kata ya Masuguru na Marumba, waliopo kwenye Wilaya ya Nanyumbu wanatafuta huduma hii ya kupata haki mbali, maana wanaishi zaidi ya kilomita 70 kutoka pale Mangaka ambapo ndipo kuna Mahakama Kuu ya Wilaya ya Nanyumbu. Hivi Serikali haioni wakati umefika sasa kuwasaidia au kuweka utaratibu wa wananchi hawa kupata haki yao karibu na makazi au maeneo wanayoishi?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia upatikanaji wa haki kwa wananchi wa Kata ya Masuguru na Marumba. Lakini napenda tu kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya hii tunafahamu ni Wilaya mpya, na katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa Mahakama ya Mwanzo ya Mang'aka na tunatambua kwamba Wilaya hii ya Nanyumbu inazo Kata takriban 18, lakini tunalitambua hili na tutajitahidi kuliweka katika vipaumbele ili wananchi hawa wa Masuguru na Marumba waweze kupata haki na wasogezewe huduma karibu zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Lipo jengo la Mahakama ya Mwanzo lilijengwa takriban miaka mitatu katika Kata ya Kirua Magharibi Wilaya ya Moshi Vijijini. Wananchi wa eneo hilo wanatembea takriban kilomita 10 kupeleka kesi zao Mji mdogo wa Himo au Moshi Mjini. Nyumba ya kuishi siyo tatizo.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka Hakimu katika Mahakama hiyo?

**SPIKA:** Swali jipya kabisa kabisa, jamani! Hebu oneni hapa! Naweza kusema lisijibiwe. Labda kwa sababu Naibu Waziri anatembea sana, aje ajibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba tatizo la ukosefu wa Hakimu katika Mahakama hii ya Mwanzo ya Kirua Magharibi tunalifahamu, lakini pia nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili.

Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa tunao mpango wa kuajiri Mahakimu Wakazi wa Mahakama za Mwanzo 300 na pindi kibali hicho kitakapotoka tutapeleka Hakimu Kirua Magharibi.



**SPIKA:** Mheshimiwa Lugola, ikiwa ni swali fupi, wengi mnapata nafasi.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Hakimu aliyekuwa Mahakama ya Mwanzo Nansimo wamemhamisha; lakini jirani karibu kilomita 12 kuna Mahakama ya Mwanzo Kenkombyo, lakini wananchi wa ile Mahakama ambapo Hakimu ametolewa wamelazimishwa wapeleke kesi zao Bunda kilomita 85 na kufungua kesi mpya Bunda ambako ni Mahakama ya Mwanzo.

Sasa nilikuwa nataka kujua, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini Mahakama ya Mwanzo iliyopo kilomita 12 isisikilize hizi kesi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba tunawapa pole wananchi wa Nansimo, na swala hili tumelipokea, lakini itabidi tulifuatilie kwa kina ni sababu gani zimepelekea huduma hii ya Mahakama ya Nansimo kupeleka katika Mahakama ambayo ipo mbali zaidi wakati ipo Mahakama karibu kama ambavyo mwenyewe umeeleza takribani kilomita 12. Tatalifuatilia ili kuhakikisha kwamba huduma hii inaweza kurudishwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali litaulizwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa niaba yake Mheshimiwa Diana Chilolo.

Na. 14

**Kiwanda cha Kuchuja Mafuta -  
Kanda ya Kati Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (k.n.y. MHE. MWIGULU L. N. MADELU)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawawezesha kujenga kiwanda cha kuchuja mafuta Kanda ya Kati Singida ili kuchochea kilimo cha alizeti?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kuhamasisha na kuhimiza Sekta ya Binafsi kuanzisha Viwanda ikiwa ni pamoja na Viwanda vya Kusindika mafuta ya alizeti katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Mount Meru Millers Ltd* hivi sasa inaboresha mitambo yake kwa kufunga mtambo mkubwa katika Mkoa wa Singida kwa ajili ya kusindika mafuta ya alizeti kwa ubora wa kiwango cha juu kabisa, yaani *double refinery*. Mtambo huo utakuwa na uwezo wa kusindika tani 800 kwa siku na mafuta yatakayozalishwa yatawawezesha wakulima wa alizeti Mkoa wa Singida wawe na uhakika wa kilimo cha alizeti na kupata mafuta yenye ubora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa yupo Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kupitia ushirika wao wa *Sokoine University Graduate Entrepreneurs Cooperative (SUGECO)* amepata mkopo toka Benki ya *CRDB* na kununua mashine ya kusindika mafuta ya alizeti kwa ubora wa kiwango cha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

juu (*double refinery*). Mashine hiyo imefungwa katika kijiji cha Ulemo Wilaya ya Iramba ambayo ipia itakuwa na uwezo wa kusindika mafuta ya kilogramu 6,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi hii mikubwa, itasaidia kuinua kilimo cha alizeti na uzalishaji wa mafuta ya alizeti katia Mkoa wa Singida na hivyo kuinua uchumi wa Mkoa wa Singida yenyewe na nchi kwa ujumla.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chilolo, swali la nyongeza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa, ujenzi wa Kiwanda hiki cha *Mount Meru* ni matunda ya swali langu la tarehe 15 Julai, 2009 na jitihada za Mbunge wa Jimbo kufuatilia. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kumshawishi Mheshimiwa Rais kwenda kuweka jiwe la msingi na hatimaye kukizindua kwa kuwa, kiwanda hiki kitakamilika mapema mwakani 2014?

La pili, kwa kuwa kiwanda hiki cha *Mount Meru* kinachojengwa na mwekezaji ni kikubwa sana, kinasemekana kitakuwa kiwanda cha kwanza kwa ukubwa Afrika Mashariki: Je, Serikali itakuwa tayari kumsimamia mwekezaji kuhakikisha vijana wa Mkoa wa Singida wanapata ajira na vijana wengine wa Kitanzania kupewa kipaumbele kuliko kuletwa wataalam kutoka nchi za nje ili waweze kupata ajira kwa urahisi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Mengine ni rahisi tu. La kwanza ni rahisi kabisa!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi nitoe pole kwa msiba mkubwa aliopata Mheshimiwa Mbunge hivi karibuni. La kwanza la kumwomba Mheshimiwa Rais awe mgeni rasmi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

katika uzinduzi, ningependa tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kushirikiana na Mkoa wenyewe wa Singida, na wenyewe Wabunge na Wizara yangu tutashirikiana tuone kwamba ifikapo Juni ambapo kiwanda hiki kitaanza majaribio ya kwanza ya mwezi Juni, 2014 na mitambo itakuwa imeshakamilika ya mwezi wa Nne mwakani, basi tuangalie uwezekano wa kuweza kumwalika Mheshimiwa Rais aweze kuzindua.

Mheshimiwa Spika, la pili, la ajira kwa vijana wa Singida, kwanza kabisa napenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, hasa yeye binafsi kwa kuzindua hoja hii tangu mwaka 2009, pamoja na Wabunge wengine ambao wanazidi kuzindua hoja hii ya kupata kiwanda cha *Mount Meru* ambacho kimejitokeza pamoja na huyo wa *SUGECO* ambaye ni mwanafunzi alikuwa anamaliza pale Sokoine.

Mheshimiwa Spika, niseme hii ni fursa kwa wananchi wa Singida, wakulima wote na wafanyabiashara wote wa Singida kwamba mchangamkie uboreshaji wa kiwanda hiki kikubwa. Endapo kitakamilika mwaka 2014, basi mpeleke mafuta yenu ambayo mmeshazalisha kwa maana ya kusindika ili yaweze kuwa *double refined* katika mitambo hii miwili ya *SUGECO* pamoja na hii ya *Mount Meru*.

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuta Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida kwa niaba yake, Mheshimiwa Mikidadi.

Na. 15

**MHE. RIZIKI S. LULIDA** aliuliza:-

Bandari ya Lindi ni moja kati ya Bandari kongwe ambayo kwa sasa haitumiki na majengo yake yamekuwa kama vichaka:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza Bandari hiyo na kurudisha hadhi yake?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Lindi kwa sasa haitumiki kutokana na tatizo la muda mrefu la mara kwa mara la kujaa mchanga kwenye eneo la Gati. Mwaka 1986, Serikali ilikarabati Gati hili kupitia ufadhili wa Serikali ya Norway kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.8. Ukarabati huo ulikamilika mwaka 1999 na ulihusisha utoaji wa mchanga kwenye bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo za utoaji mchanga, mradi huo haukudumu kwa muda mrefu kutokana na mchanga kuendelea kujaa kwa kasi eneo la gati. Uchunguzi uliofanywa na kampuni ya ushauri ya *Hamburg Port Consultancy* ya Ujerumani mwaka 2007, ulipendekeza hatua mbili kuchukuliwa ili kudhibiti hali hiyo. Moja, kujenga gati katika eneo lingine au ya pili, kulifanyia ukarabati gati la sasa ili kuliongezea urefu kutoka ufukweni kuelekea baharini kwa mita 100.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili la ripoti ya uchunguzi la kuongeza urefu wa gati kwa mita 100 ya ndani ya maji, lilionekana kuwa muafaka zaidi. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013 kiasi cha Shilingi bilioni mbili kilitengwa kwa ajili ya kazi hii, na hivyo zabuni kutangazwa, lakini hakuna mzabuni aliyejitokeza kufanya kazi hiyo, kwa kiasi hicho cha fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya zabuni hiyo kushindikana, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari katika mwaka wa fedha 2013/2014 imeutangaza tena mradi huo, kwa ajili ya kumpata mwekezaji atakayefanya usanifu wa kina, pamoja na ujenzi wa Bandari ya Lindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mikidadi, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Bandari ya Lindi ni bandari iliyokuwa inatumika Kanda ya Kusini nzima; Mtwara, Ruvuma na Lindi na sehemu nyingi za Kanda ya Kusini. Lakini imekufa kabisa. Watu wa Norway walitengeneza au kukarabati Mradi huu kwa miaka 13 hawakuweza na mpaka leo haujafanya kazi. Sasa hivi takribani miaka inapata 137 haijaweza kutumika, haijaweza kutengenezwa tena.

Mheshimiwa Spika, ni Wajerumani peke yake ambao waliweza kutumia Bandari hii ikafanya kazi Kanda ya Kusini. Je, kwanini Serikali isipate nafasi au muda wa kwenda kuwauliza wenzetu Wajerumani waliitumiaje Bandari hii? Wakati ule wanahamisha mjusi kutoka Tanzania kwenda Ujerumani walitumia Bandari ya Lindi? Tunaomba sana Serikali ifanye hivyo. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Akisimama Mheshimiwa Mikidadi, mjusi lazima atakuwemo tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Bandari ya Lindi sasa hivi haitumiki kwasababu kimsingi kabisa imejaa mchanga. Meli yoyote haiwezi kutia nanga pale na utafiti umefanywa mara kadhaa, sio mara moja wala mara mbili, ukihusisha wataalamu wa ndani na wa nje ya nchi, kuhusu namna bora ya kukarabati sehemu hiyo na mapendekezo yametolewa kama nilivyoyasema kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Spika, wazo la kwenda Ujerumani kuwauliza wenzetu wale walifanyaje miaka ile, nalipokea, lakini sioni kama kuna sayansi mpya pale katika kutafiti nini sababu ya mchanga kujaa pale. Sababu ya kujaa mchanga kwenye Bahari ya Lindi inafahamika. Sasa hivi tu kinachotakiwa ni kuchukua hatua. Hatua ya kwanza iliyopendekezwa ilikuwa ni kujenga. Mwaka 2012 tulitangaza zabuni, hakujitokeza mtu. Angejitokeza mtu ujenzi ule wa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]

kuongeza mita 100 ungekuwa umefanyika. Lakini hakujitokeza mtu, kwa hiyo, ndiyo maana tumetangaza tena, tunatarajia *this time* atapatikana Mkandarasi ili tuweze kujenga hiyo Bandari ya Lindi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwangalie na saa, kwani muda umekwisha sana. Ninayo matangazo kidogo, matangazo na wageni sina, lakini ningependa kutoa taarifa kwamba tutakuwa na Kamati ya Uongozi mara baada ya kikao, kama saa tano hivi. Kamati ya Uongozi ni Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge. Naona rafiki zetu kule asubuhi wanasema Bunge halina ratiba, haikufanya kazi. Siyo kweli, tuna utaratibu wetu. Mkutano huu toka mwanzo tumesema utahusika zaidi na taarifa za Kamati.

Sasa tunachojaribu kukutana Kamati ya Uongozi ni kupanga Kamati zipi zitakuja lini? Hiyo ndiyo shughuli tunayofanya. Wakati huo huo Kamati zote zinatakiwa kuwa na Taarifa zao zikiwa zimechapwa na kupelekwa kunakohusika, kwasababu na wenyewe wataweka *on the table* kama ilivyo ada.

Kwa hiyo, siyo kweli kwamba hatukuwa na ratiba. Tuna ratiba, na Bunge hili ni rasmi kwa ajili ya Kamati isipokuwa Muswada mmoja tu wa *referendum* ndiyo utabidi uje kwasababu ya umuhimu wake. Vinginevyo, kazi kubwa itakuwa ni ya Kamati. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba hatuna ratiba, tunayo isipokuwa ni namna ya kujipanga.

Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi itakuwa na kikao kama saa 5.00, halafu jioni tutakuwa na kikao chetu cha kawaida cha *briefing* kuhusu hali halisi tuliyonayo ndani ya nchi, sisi wenyewe na wafanyakazi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, saa 10.00 wote mnatakiwa kule Ukumbi wa Pius Msekwa, huo ndio utaratibu. Kwa hiyo, tunazo kazi za kufanya.

Waheshimiwa Wabunge, kati ya kipindi tulichomaliza Bunge lililopita mpaka Bunge hili tumepata misiba miwili.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Kwanza kabisa Mheshimiwa Diana Chilolo amefiwa na mama yake; tena alifiwa nadhani hata hamjasafiri kwenda mbali, ndiyo msiba wa mama yake ukatokea. Najua kuna wengine pia wamefiwa, tutaambiwa kwenye Kamati ya *Briefing*. Wakati huo huo siku ile tunaahirisha kikao, Mtumishi wetu ambaye wengi mnafahamu, Anselm Mrema, alikuwa Msaidizi katika Shughuli za Bunge hapa, mnamfahamu sana, kijana mmoja alikuwa mpole sana, mfanyakazi mzuri sana alifariki ghafla. Kwa hiyo, yule kijana hatunaye, tumemzika nyumbani kwao Kilaracha. Kwa hiyo, nawaombea tu Mwenyezi Mungu awape mapumziko mema huko Mbinguni. Baada ya kusema hayo, sasa namwita Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni 64 (1) (c), ya kwamba: “Mbunge bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba, inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo, na majadiliano katika Bunge; Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri maamuzi ya Mahakama.”

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa kilichotokea Bungeni mapema, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali Na. 11 lililohusu kupanua wigo wa kodi ili kukusanya mapato kwa wingi; na wakati anajibu swali la kiwango cha mapato ya ziada kilichokusanywa, akazungumzia kuhusu Shilingi bilioni 81 ambazo hazijakusanywa kwasababu ya kesi iliyopo Mahakamani kutokana na suala la ushuru wa bidhaa ya kodi ya kadi za simu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali hili, alichukua tahadhari mwanzoni kwa kusema kwamba hatazungumza kwa kirefu kwasababu jambo hili lipo Mahakamani. Lakini baadaye akazungumza kwa maana ya kuelezea umuhimu wa ile kodi, ulazima wa ile kodi na uzuri wa ile kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako, sisi Wabunge wengine tulliandikia Ofisi yako tukiomba fursa ya kuelezea ubaya wa ile kodi. Hatukupewa nafasi kwa



## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

sababu tuliambiwa jambo lipo Mahakamani. Lakini Serikali inapokuja suala la kuelezea uzuri wa hiyo kodi, inapewa nafasi ya kuzungumza hapa Bungeni.

Siyo katika jambo hili tu, wengine tumeleta maswali, kwa mfano, mgawanyo wa fedha za *DECI* ambazo zipo kwenye Wizara hii ya fedha. Tuliambiwa kwamba Wizara ya fedha haiwezi kujibu kuhusu mgawanyo wa fedha za *DECI*, ambazo Serikali ilikusanya Shilingi bilioni 14, kwasababu kesi ipo Mahakamani. Lakini inapokuja maswali ya Wizara, Wizara inazungumzia mambo yaliyopo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ningeomba mwongozo wako ama Mawaziri wakemewe waache kabisa kuzungumzia mambo yaliyopo Mahakamani, ama kama ni halali kwa Mawaziri kuzungumzia mambo yaliyopo Mahakamani, basi na sisi Wabunge tupewe nafasi ya kuzungumzia mambo yaliyopo Mahakamani bila kuingilia uhuru wa Mahakama ambayo ni jambo sahihi kabisa kwa mujibu wa *Common Wealth Parliamentary Practise*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika na wewe unajua kabisa unachokisema ndivyo unavyosema. Unajua kilichotokea, Mheshimiwa Waziri mimi nimemsikiliza, amesema toka mwanzo kwamba hii kesi ipo Mahakamani. Kwa hiyo, siwezi kuzungumza. Ubaya wa ile kodi tulitaja humu Bungeni na ndiyo tulipitisha. Kwa hiyo alirudia kile kilichosababisha tupitisha, hakuingia kwenye Mahakama. (Makofi)

Vile vile ni marufuku kuzungumza masuala yoyote yaliyopo Mahakamani, ila mtu anasema kwamba hili suala jamani siwezi kuendelea zaidi. Ndiyo maana sikupenda kuendelea na maswali ya nyongeza kwasababu alishasema ipo Mahakamani. Kwa hiyo, ni sahihi tu.

Mheshimiwa Haji nimekuona umesimimama.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naomba mwongozo wako kupitia kanuni 68 (7) naomba nisisome.

**SPIKA:** Isome.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Niisome?

**SPIKA:** Isome ndiyo.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** He! Makubwa!

Mheshimwa Spika, kanuni ya 68 (7) inasema: "Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama mahali wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema, na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge. Majibu ya Spika yatatolewa papo hapo ama baadaye kadri atakavyoona inafaa." (*Kicheko*)

**SPIKA:** Sasa niambie tu.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Spika, nakwambia katika swali Na. 11 la Mheshimiwa Tauhida, Mheshimiwa Waziri alipojibu hili swali, katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati aliloulizia kuhusu hilo jambo lililokuwa Mahakamani ambalo mimi sitaki kulisema, aliongea kwamba kuna kodi zinazotowwa na Makumpuni ya Simu pasipo na wananchi wenyewe kujua, wala kuwa na kibali.

Kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri ni kana kwamba jambo hili amelihalalisha kwa Makampuni hayo ya simu, kwamba wanachokifanya ni sawa. Kuendelea kutozwa hizo kodi ambazo wananchi hawajui, Mheshimiwa naomba mwongozo wako, jambo hili kweli linafaa?

**SPIKA:** Nyie wandugu, kwanza kabisa kama hamjaridhika na maswali ya Mawaziri wakati wanajibu, utaratibu wake ni tofauti. Kwasababu kama tukitumia nafasi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

kuanza kusema kwamba mimi sikuridhika, sikuridhika maana yake hata Mheshimiwa Machali hajaridhika, nimemwambia tuonane ofisini. Kwa hiyo, mkitumia muda huu, basi tutakuwa hatufanyi kazi zinazostahili. Majibu yaliyotolewa yalitolewa, kama wewe una mashaka na majibu yale niandikie mimi, nitakwambia namna ya kufanya. Lakini hatuwezi kuanza kubishana hapa, mimi sijui kama alivyosema ni sahihi ama sivyo, na siyo kazi yangu kujua. Kwa hiyo, utaniandikia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwamba tulivyosema leo tutafanya hizi kazi mbili, kwanza Kamati ya Uongozi halafu baadaye Wabunge wote mtakwenda kule Pius Msekwa. Naomba muwahi tuweze kupata *briefing* ya mambo mbalimbali.

Kwasababu hiyo basi, kesho tutaendelea na ratiba kama itakavyokuwa imepangwa na Kamati ya Uongozi. Mwenendo wote wa kazi zetu lazima Kamati ya Uongozi itoe kibali. Hatuwezi kwenda vinginevyo.

Kwa hiyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.55 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya  
Jumatano, Tarehe 4 Desemba, 2013  
Saa Tatu Asubuhi)*